OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

HALMASHAURI YA MANISPAA TEMEKE

Kijichi Shule ya Sekondari,

S.L.P. 41463,

DAR ES SALAAM.

YAH; MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIJICHI WILAYA YA TEMEKE MKOA WA DAR ES SALAAM. MWAKA 2021

MAWASILIANO: 0655406444 AU 0653282261

JINA LA MWANAFUNZI _____

NAMBA YA FOMU _____

Nafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Hongera sana!

Shule ya Sekondari Kijichi ipo umbali wa Km 8.9 kutoka makao makuu ya Wilaya ya Temeke. Shule ipo katika Kata ya Kijichi jirani na maghorofa ya polisi.

Usafiri wa basi unapatikana kutoka eneo lolote. Panda daladala za Mbagala kuu au Kijichi, shuka kituo cha **kijichi ccm**, kisha chukua bodaboda (pikipiki) hadi shuleni.

Mhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11 /01/2021 unatakiwa kuripoti tarehe 11/01/2021 saa moja kamili asubuhi, na mwisho wa kuripoti ni wiki sita kuanzia tarehe ya kuripoti.

1. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

i) SARE YA SHULE

S/N	WAVULANA	WASICHANA
1	Suruali mbili (2) za damu ya mzee **Zingatia rangi halisi ya kitambaa**	Sketi mbili (2) za damu ya mzee, ziwe ndefu zinazofunika magoti – mshono uwe rinda box. Angalia mchoro hapo mbele (uk.2). **Zingatia rangi halisi ya kitambaa**
2	Mashati mawili (2) meupe yasiyobana au mafupi au makubwa sana (mashati hayo yawe aina ya tomato)	Mashati mawili (2) meupe yasiyobana au mafupi au makubwa sana (aina ya tomato) Au Nusu kanzu nyeupe ndefu isiyobana na hijabu nyeupe isiyo na urembo wowote (**hijabu ni lazima ifunike makalio)**
3	Soksi nyeusi jozi mbili (2),kuvaa soksi ni lazima	Soksi nyeupe jozi mbili (2)
4	Viatu vyeusi vya ngozi visivyochongoka mbele, visivyo na urembo. Viatu vinavyoruhusiwa ni vya kufunga na kamba.	Viatu vyeusi vya ngozi visivyochongoka mbele, visivyo na urembo. Viatu vinavyoruhusiwa ni vya kufunga na kamba
5	Mkanda mweusi wa ngozi usio na urembo (mkanda wa kitambaa hauruhusiwi)	

SARE ZA MICHEZO

S/N	WAVULANA	WASICHANA

01	Fulana na bukta (rangi ya blue)	Fulana na sketi iliyounganishwa na bukta (rangi ya blue)
02	Raba nyeupe na soksi nyeusi (rangi nyingine haziruhusiwi)	Raba nyeupe na soksi nyeupe. (rangi nyingine haziruhusiwi)

VIFAA VYA MASOMO

(a) Madaftari makubwa (counter book) Quire 3 au 4.
(b) Mathematical set.
(c) Begi la shule la kubeba mgongoni.
(d) Peni na penseli.

(NI LAZIMA KUJA NA NAKALA YA CHETI CHA KUZALIWA)

2. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yoteinayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa (**muda wa kufika shuleni ni saa 06:45 asubuhi).**
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Nilazima kila mwanafunzi aweke rank kwenye shati la shule kulingana na kidato anachosoma kwenye bega la **kushoto**
j) Kutunza mali za umma **(ukiharibu mali za shule kama vile dawati au kiti utalazimika kuzilipa bila usumbufu wowote ule)**

3. VITU VISIVYORUHUSIWA SHULENI

1. Pete
2. Kunyoa nyusi
3. Hereni
4. Kupaka hina
5. Rangi za kucha
6. Kucha ndefu
7. Kupaka piko (rangi nyeusi) kwenye nywele/upara
8. Kukali au kurilax ni marufuku
9. Hairuhusiwi kunyoa mtindo wowote
10. Hairuhusiwi kunyoa upara
11. Hairuhusiwi kuvaa mabuti au viatu vinavyofanana na jeshi
12. Hairuhusiwi kuvaa sandozi, mikanda isiyoendana na vazi la shule
13. Mashati makubwa sana na slim fiti hayaruhusiwi. **Pamoja na suruali za modo (zinazobana) ukikamatwa na kosa hili suruali itakatwa na utasimamishwa shule. Hapa mzazi atawajibishwa kwa uzembe.**
14. Simu ya mkononi hairuhusiwi. Ukikamatwa na simu utanyang'anywa na kusimamishwa shule.
15. Hairuhusiwi kuja na redio shuleni
16. Hairuhusiwi kuja na "game" shuleni
17. Hairuhusiwi kuja na CD au Flash shuleni

4. SHERIA KWA UJUMLA

Kila wakati fikiri kwanza kabla ya kunena na tumia busara kutenda.

5. ADHABU

i) Adhabu zinaweza kutolewa na mwalimu yeyote kwa mwanafunzi anayeonyesha utovu wa nidhamu
ii) Kiranja pia anaruhusiwa kutoa adhabu kulingana na kosa lililotendwa na mwanafunzi, ilimradi asipige viboko au kuzuia kuingia darasani wakati wa masomo.

iii) Kosa linapokuwa kubwa litaandikwa katika jalada la mwanafunzi na kitabu cha kumbukumbu za makosa (**black book**). Akiandikwa katika kitabu cha kumbukumbu za makosa ya wanafunzi anaweza **kufukuzwa shule**.

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule au kusimamishwa shule moja kwa moja.

1. Wizi
2. Uasherati au ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau bendera ya Taifa
8. Kuwa mjamzito au kupata mimba
9. Kuoa au kuolewa
10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule na watu
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Kuwa na simu ya mkononi bila ruhusa.

6. MWENENDO MWEMA NA NIDHAMU

1. Msalimu mwalimu kwa heshima wakati wowote unapokutana naye hasa kwa mara ya kwanza kwa siku hiyo.
2. Mwanafunzi asimame wakati Mwalimu ama mtu yeyote anayemzidi umri anapita au kuingia darasani
3. Usizungumze na Mwalimu ama mtu yeyote anayekuzidi umri wakati umeweka**mikono mifukoni ama umevaa kofia kichwani au ukiwa umevaa miwani ya jua au kutafuna kitu mdomoni**
4. Usibishane na Mwalimu au kiongozi yeyote. Uamuzi wa Mwalimu ni wa mwisho.
5. Usipige kelele, fujo au ghasia katika sehemu zinazohitaji ukimya kama vile **darasani, maabara, maktaba na kwenye gwaride**
6. Usiwe mchafu kimwili au kimavazi, uwe na nywele fupi bila kunyoa kipara (hairuhusiwi kuwa na ndevu au masharubu)
7. Usitumie sigara, bangi na madawa ya kulevya pamoja na pombe.
8. Timiza wajibu au kazi uliyopangiwa.
9. Mwanafunzi haruhusiwi kubeba madaftari mkononi (**madaftari ni lazima yawekwe kwenye mabegi)**
10. Usitumie lugha ya matusi, na kusuka mitindo isiyokubalika (misuko inayokubalika ni**utii wa Roda mistari 5, 7 na 9)**
11. Onyesha heshima kwa walimu, raia na wengine wote
12. Usiende kwenye vilabu vya pombe au baa hata kama hunywi pombe na hata kwenye magesti.
13. Usiandike mahali pasipohusika kama vile kutani, vitabuni, kwenye samani za shule n.k (ukikamatwa na kosa hili utalipishwa kupaka rangi).
14. Usimpige au kumshambulia mwalimu, mwanafunzi mwenzako ama hata mtu mwingine yeyote.
15. Usikatae uteuzi wa kushiriki shughuli mbalimbali kama vile michezo, maandamano, uwakilishi **(uongozi)** n.k
16. Usichelewe kurudi shuleni wakati wa likizo na usipitishe siku za ruhusa ya kuwa nje ya shule. Mwanafunzi akikosa kuhudhuria shule zaidi ya siku tatu mfululizo atalazimika kufika pamoja na mzazi/mlezi wake aliyemwandikisha.
17. Usigune au kuzomea wakati mwalimu au kiongozi yeyote anapotoa matangazo au hotuba
18. Usibandike tangazo lolote bila ruhusa ya Mwalimu anayehusika na tangazo husika.
19. Hotuba zote lazima zionwe na Mkuu/Makamu wa shule, kabla ya kutolewa katika hadhara husika.
20. Usifanye mkutano bila ruhusa ya Mwalimu anayehusika kukilea kikundi kinachohusika.
21. Usihubiri dini, siasa au jambo lolote. Sala zote zifanyike mahali panapohusika kama vile kanisani au msikitini.

MAJUKUMU YA MZAZI/MLEZI

Mzazi/mlezi anahusika na majukumu yafuatayo:

1. Sare za shule na michezo
2. Vifaa vya kujifunzia vikiwemo: madaftari 11 (yawe quire 3 au 4), kalamu, begi n.k
3. Chakula kwa mwanafunzi wa kutwa
4. Matibabu
5. Nauli ya kwenda shuleni na kurudi kwa wanaotumia usafiri

6. Kufuatilia maendeleo ya mwanao na tabia yake kwa ujumla. Ikiwemo kuchukua ripoti kwa kila mwisho wa mhula.**Ukiacha kuchukua ripoti ya mwanao kwa muda uliopangwa itapelekwa ofisi za Kata/Polisi na utaichukulia huko kwa adhabu kali.**
7. Mahitaji mengine ya kibinadamu kwa wasichana na wavulana.
8. Mzazi/ mlezi ni lazima akague madaftari ya mwanae ili kujua kuwa huwa anaandika darasani au vinginevyo. Ukikuta kuna tatizo wasiliana na walimu.

Mzazi kama sehemu ya wananchi na jamii inayoizunguka shule, watashiriki katika kazi za ujenzi wa miundo mbinu ya shule kwa kuchangia nguvu zao au fedha kadri itakavyoamuliwa na Mtaa, Kata, Tarafa au Halmashauri husika.

FOMU YA KUANDIKISHWA SHULE YA SEKONDARI KIJICHI

A: IJAZWE NA MWANAFUNZI HUSIKA

1. Jina kamili la mwanafunzi(**litumike jina lililo katika TSM 9**) …….…….
2. Kabila …….....……..
3. Uraia..…….…
4. Dini….……...…….....
5. Tarehe ya kuzaliwa .....……...…..…
6. Shule ya msingi aliyosoma …… Kata ……
7. Tarehe ya kuhitimu shule hiyo ……....……..

Picha ya mwanafunzi

B: MAELEZO BINAFSI YA MZAZI/MLEZI:

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi ……
2. Anwani kamili mjini Dar es Salaam ……..……
3. Sehemu unayoishi ……..……
4. Mtaa …….……..
5. Namba ya simu ya mwenyekiti wa serikali za mtaa **(LAZIMA)** …….……..
6. Nambari ya simu ya Mzazi/Mlezi ……...……..
7. Namba ya simu ya ndugu wa karibu …….……

Picha ya mzazi

Picha ya mzazi

C: MAELEZO YA KIKAZI YA MZAZI/MLEZI

1. Jina la mwajiri na Idara ……...
2. Anwani yake …….....……..
3. Namba ya simu ……
4. Kazi ya Mzazi/Mlezi …..…….

D: MDHAMINI WA MWANAFUNZI (AWE YEYOTE AMBAYE ANAWEZA KUTOA TAARIFA ZA MWANAFUNZI ALIYETAJWA HAPO JUU)

1. Jina la Mdhamini …….
2. Anwani yake ……..……..
3. Namba ya simu ya mdhamini ……..……
4. Mahali anapoishi mdhamini .....……..

E: SOMO LA DINI

Mimi ……. ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi ……..kidato cha …… Ninamruhusu mtoto wangu kuhudhuria somo la Dini ya…….…… Dhehebu la ……. Siku ya Jumatano akiwa shuleni Kijichi

Sahihi ya Mzazi/Mlezi …… Tarehe ……

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

STATION …….

DATE ……

PART: A

To
Medical officer
……..
……...
Miss/Mr …….
Please examine the above named as to his/her fitness for admission as student at Kijichi Secondary School in the following common diseases/problems
Put tick for positive and a cross for negative in a box provided

Pregnancy	
Asthma	
Diabetes	
Worms (stool)	
Epilepsy	
TB (Tuberculosis)	
Sickle cell	
Heart disease	
Yellow Fever	
U.T.I	
Malaria	

PART B:
MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Medical Officer)
I have examined the above named and consider that she/he is physical FIT/UNFIT for admission at Kijichi Secondary School

DATE …… SIGNATURE ……..

STATION ……. DESIGNATION ……..…

OFFICIAL STAMP

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIJICHI
Mkuu wa shule
Shule ya Sekondari Kijichi
DAR ES SALAAM

Mimi: Mwanafunzi …… (jina kamili)
Nimekubali nafasi niliyopewa ya kuingia kidato cha ……. Mwaka ……..
Katika shule ya Sekondari Kijichi. Naahidi kwamba;

1. Nitatii sheria zote za shule kama nilivyozisoma
2. Nitatia bidii katika masomo, kazi na shughuli zote za shule
3. Nitashiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali, kuzalisha mali iliyobora bila kuitia hasara shule kwa kuharibu au kupoteza mali ghafi (raw material) ya kuzalisha mali.
4. Nitakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali ya juu, mkakamavu na mwenye mwenendo safi wakati wowote hata nikiwa nje ya shule kwa madhumuni ya kuipa na kutunza sifa ya shule ya Sekondari Kijichi.

MUNGU NISAIDIE
Sahihi ya Mwanafunzi…… Tarehe ……..

KWA MZAZI / MLEZI
Mimi (jina la Mzazi/Mlezi) ……

Mzazi/ Mlezi wa ……..naahidi kwamba:-

1. Nitampatia mwanangu mahitaji ya shule kama yalivyotajwa katika maelekezo ya kujiunga na shule.
2. Nitakuwa tayari kutoa msaada wowote utakapohitajika na mwalimu (maoni, adhabu) katika kumlea mwanangu.
3. Nitamhimiza mwanangu kufanya mazoezi yake ya masomo nyumbani (home work) na kufuatilia maendeleo yake na tabia yake shuleni.
4. Mwanangu akiwa nyumbani nitamtunza na kumwangalia vizuri kuhusu mwenendo wake.
5. Nitakuwa tayari **kupelekwa kwenye vyombo vya dola** kama sitatoa ushirikiano na walimu shuleni kama vile **kutohudhuria vikao mbalimbali, kutokuchukua ripoti ya mwanangu n.k.**
6. **Form ya kupima afya ya mwanafunzi ujaze kutokana na majibu ya vipimo. Hakikisha haina vipimo vya kugushi.**

NB: Nitawasiliana na uongozi wa shule, walimu na walezi kuhusu mwenendo na maendeleo yake kitaaluma na kitabia.
Sahihi ya Mzazi/Mlezi_____

Namba ya simu ya mzazi/mlezi……

Tarehe ……..

Jina la eneo unaloishi: ……..

Jina la mwenyekiti wa Mtaa: ……

Namba ya simu ya Mwenyekiti wa Mtaa: ……